# ***BANDA LA KULELEA VIFARANGA :***

Ukipenda kujenga nyumba ya vifaranga itafaa ufikirie yafuatayo:-

Nyumba ya vifaranga iwe karibu na nyumba yako mwenyewe ili uweze kuwakagua vifaranga wako mara kwa mara.

Ijengwe hatua 20 au zaidi mbali na nyumba ya kuku wakubwa, hii ni kinga mojawapo ya kupunguza hatari ya maambukizi ya magonjwa.

Nyumba ya vifaranga isiruhusu ubaridi au unyevu au wanyama waharibifu kuingia. Lakini nyumba iingize hewa na mwanga wa kutosha kila wakati.

Nyumba iwe na eneo la kutosha ili vifaranga wapate nafasi ya kutembea kutafuta chakula na maji bila kubanana.

Ijengwe kwenye sehemu isiyoelekea upepo unaotoka kwenye nyumba ya kuku wakubwa. Tahadhari hii husaidia vifaranga kuepukana na magonjwa yanayoenezwa na

upepo

.



ENEO: Vifaranga hawahitaji eneo kubwa katika muda wa majuma 4 ya kwanza. Nafasi inayohitajiwa kwa kukadiria ni meta za eneo 1 kwa kila vifaranga 16. Kwa mfano nyumba yenye Meta 10 za mraba

inatosha kulea vifaranga 160 hadi umri wa majuma 4. Vipimo vya nyumba yenye eneo kama hili inaweza kuwa na hatua 5 kwa hatua 4 au hatua 3 kwa 3.25. Utajenga kutegemea na eneo ulilonalo. Baada ya majuma 4 ya umri ongeza nafasi na uwape vifaranga eneo la kuwatosha.

SAKAFU: Sakafu nzuri katika nyumba ya vifaranga ikiwezekana inafaa ijengwe na simenti iliochanganywa na zege. Ili kupunguza gharama, unaweza kutumia vifaa vya ujenzi vinavyopatikana kirahisi katika eneo lako vitumikavyo kusiriba sakafu kama udongo wa kichuguu au unaweza kulainisha kinyesi cha ng’ombe kwa maji na kusiriba eneo lote la sakafu.

UKUTA: Ingefaa kuta za nyumba za kulea vifaranga za matofali, udongo, mabati au debe. Kuta za matofali na udongo zipigwe lipu ili kurahisisha

usafishaji wa nyumba au umwagiaji wa dawa. Urefu wa kuta uwe tangu meta 1.8 – 2.4 (futi 6-8). Sehemu ya kutoka chini ya meta 0.9 – 1.2 (futi 3 – 4) izibwe na ukuta wa tofali au udongo na sehemu ya juu iliyobakia yenye meta 0.9 – 1.2 (futi) 3-4) ijengwe kwa wavu wa chuma au fito.

MBAO: Nguzo za miti au mbao zilowekwe dawa ya mbao kama vile "Dudu killer" au oili chafu ili kuzuia kuoza. Ukitumia miti ni vizuri uondoe magome ambayo yanaweza kuweka vimelea na wadudu.

MADIRISHA: Unaweza kutumia maboksi, mikeka ya magunia, mapazia ya magunia ni rahisi na yanaweza kuwekwa kwa kupigiliwa misumari kwenye dari na upande wa chini pazia ipigiliwe misumari kwenye ubao ili ininginie.Unaweza kukunja mapazia/magunia ili uingize hewa na mwanga wa kutosha katika nyumba ya vifaranga.

PAA: Mjengo wa paa uwe unaoweza kuwapatia vifaranga hewa ya kutosha hivyo paa liwe na tundu la kutoa nje hewa yenye joto. Kwa kadri utakavyoweza, unaweza kutumia madebe, mabati, makuti au nyasi n.k. kuezeka nyumba ya vifaranga. Sehemu ya paa ikianza kuvuja iezekwe bila kuchelewa

## ***ULEAJI WA VIFARANGA***



Watu wengi wamekuwa wakifeli na kukata tamaa kwa kukosa uwezo na uelwa sahihi wa namna ya kulea vifaranga kwa maanamtu anachukua bila ABCD… za vifaranga. Ili ufanikiwe kuwakuza vifaranga sio kazi ngumu wala sio kazi nyepesi, ni vile tu kuwajulia jinsi ya kwenda nao vizuri. Malezi ya Vifaranga yanaanzia mbali sana tofauti na wengi wanavyofikiria, watu wanachukulia malezi ya vifaranga ni kuanzia vifaranga wakitotolewa, kitu ambacho sio kweli, malezi ya vifaranga yanaanzia kwa mama mtagaji. Ili ufanikiwe kuwalea vifaranga lazma uzingatie yafuatayo;

1. Mama asiye na magonjwa, watu wengi hawajui lakini ndo ukweli kwani kunayo baadhi ya magonjwa yanaambukuzwa toka kwa mama mtagaji wa yai, hata kama utatumia njia gani za kutotolesha lakini kama wale watagaji wana magonjwa basi ni rahisi sana kuwaathiri mpaka vifaranga watakaotokana nao. Mfano kama mama ana mafua sugu ni vigum sana kwa kifaranga chake kuishi .

2. Maandalizi kabla ya kupokea vifaranga, kabla hujaingiza vifaranga kwenye eneo lako unalotegemea kuwatunzia lazima uwaandalie vizuri kwa kuhakikisha huduma za msingi zinakuwepo na ni salama. Ili upokee vifaranga lazma kama unapotaka kuwatunzia palishawahi kutumika uhakikishe panasafishwa ili kuua wadudu/ visababishi vya magonjwa vinavyoweza kusababishwa au kuambukizwa toka kwa wale waliokuwepo awali. lazima pasafishwe kwa dawa ili kuuwa mabaki na kupafanya pawe salama. Pia

inapendekezwa kabla ya kuwaingiza hakikisha kwa chanzo cha joto ulichonacho unawawekea joto la kutosha kwano vifaranga wanahitaji joto muda wote.

3. Joto, vifaranga wanahitaji joto muda mwingi hivyo kulingana na uwezo na mazingira uliyonayo unapaswa kuwapatia joto kwani hata wakiwa na mama yao muda mwingi wakiwa na baridi mama yao huwafuniaka na mbawa zake ili wapate joto. Lengo la joto ni kumtengenezea kifaranga uwezo wa kuwa timamu muda wote make akiwa na badiri kudorola na kudhoofika huwa vyepesi na mwishowe hufa.

4. Ubora wa banda, malezi sahihi ya vifaranga yanahusisha makazi sahihi ya vifaranga. Makazi ya banda lazima yamkinge kutokana na maadui wa


aina mbali mbali ikiwa ni pamoja na mazingira hasa baridi, wadudu kama panya, utitiri, digidigi, na wengine wanaopatikana katika mazingira ya mfuagaji, pia banda bora lazima liwe na miundombinu sahihi ya namna ya kulisafishwa bila kuathiri maisha na ustawi wa hifaranga kwa mfano kwa kuwalelea kwenye cages au hata banda lenye wavu kwa chi linalozuia vifaranga kula uchafu na kinyesi chao nk.



5. Chanjo na madawa, kumekewa na wimbi kubwa la mahubiri ya matumizi ya dawa za asili kwa ajili ya malezi ya vifaranga kitu ambacho ni sahihi lakini

bado tunakichukulia juu juu bila kinga ndani na kuangalia ukweli na uhalali wake. Msisitizo wangu ni kwamba vifaranga wapate dawana chanjo zilizopita kwenye maabara na sio zinazotolewa kwa kuhisia. Kama unataka kuwapa miti shamba wape kama ziada kwani hakuna vithbitisho vya kitaalamu vya uwezo, vipimo/viwango, ratiba na mambo mengine yote ya muhimu kwenye matumizi ya dawa.

6. Bluda, vifaranga inabidi waandaliwe sehemu yao ya kuwalelea ambayo haina kona kwa maana vifaranga huwa wanakawaida ya kupenda kukimbilia kwenye kona na kujirunda sehemu moja na mwishowe huwa wanauwana lakini ukiwatengenezea bluda utaepuka hilo kwa maana bluda halina kona hivyo kufanya vifaranga wasambae sawa maeneo yote. Pia bluda ni zuri kwa kuhihadhi joto kwani huzuia upepo ambao ungeweza kuleta ubaridi kwani upepo huondoa joto lililotengenezwa na kuleta hewa nyingine ya nje.






7. Chakula na maji, katika malezi ya vifaranga ni vizuri kuzingatia chakula kinachoendana na vifaranga wako kwani kinakuwa na mchanganyiko unaokidhi mahitaji ya vifaranga wako na pia texture yake itaendana na vifaranga kwani zhakula cha vifaranga ni laini Zaidi. Pia chakula lazma wapewe

kwa kiwango stahiki maana sio unawapa kingi sana unaweza kusababisha matatizo mengine kama chick pastig. Pia ikumbukwa kuwa mlo bora ndo nguzo ya maishabora kwa vifaranga.



8. Usafi, hakikisha banda /bluda au eneo unalolelea vifaranga wako ni safi ili kuepuka maradhi kwa maana Zaidi ya 75% ya magonjwa ya kuku hutokana na uchafu na mlo hivyo hakikisha vifaranga wako wapo kwenye eneo safi muda wote ili kuepuka kula chakula chenye kinyesi chao au kunywa maji yenye kinyesi chao kwani huweza kusababisha magonjwa

hatari kwa vifaranga kama vile coccidiosisambayo huuwa sana vifaranga.



9. Uvumilivu wa vifaranga, pia kama mfugaji lazma ujue kuwa uwezo wa kifaranga kuvumilia matatizo ni mdogo sana hivyo unalazimika kumjali kwa kila mahitaji yake ya msingi na kumuongole hatari zote anazoweza kukutana nazo kama vitu mumuangukia nk



10. Mwingiliano, vifaranga hawana uvumilivu na uwezo wao kuimili magonjwa ni mdogo hivyo jiepusha na kuwachanganya vifaranga na kuku wakubwa au unapotoka kutoa huduma kwa wakubwa badili mavazi esp viatu ili kama kuna kibaya ulichotoka nacho huko kisiingie kwa wadogo. Pia pamoja na muingiliano wa wafugaji wenyewe kutoka na kuingia kwenye mabanda yako kua sio vizuri lakini pia nashauri vifaranga wasiwekwe kwenye maeneo ya karibu na kuku wengine wakubwa kwani magonjwa mingine yanaambukizwa kwa hewa.

Kwa kuhitimisha ni kuwa idadi ya kuku watakaokuwa toka kwenye vifaranga ni lazma itategemeana na idadi ya vifaranga vyako na

matunzo ulovipa. Usipovijali vifaranga hata idadi ya wakubwa pia usijali kwani kinachotoka kinategemeana na ulichokiingiza.

……………….***MWISHO***………………

**KWA MAHITAJI YA YA HUDUMA ZIFUATAZO**

- ✓ Vifaranga siku,wiki na mwezi aina zote
- ✓ Mayai ya kuku ya kutotoleasha aina ya SASSO na KROILER
- ✓ Usimamizi wa mradi wa ufugaji kuku
- ✓ Ushauri Zaidi juu ya ufugaji

- ✓ Uandishi wa mchanganuo biashara ya ufugaji
  - ✓Utafutaji wa masoko ya ufugaji.
- ✓ Vifaranga vya bata vya siku moja
- ✓ Mayai ya bata kwa ajili ya kutotolesha

**WASILIANA NAMI KWA MAWASILIANO**

NAMBA ZA SIMU: 06564469991 Tigo

0620765518 Halotel

BARUA PEPE : Godwinmbwambo111